



TAARIFA KWA WACHANGIAJI DAMU JUU YA MAGONJWA YA KUAMBUKIZWA KUPITIA UONGEZWAJI WA DAMU

Kuna magonjwa/maambukizi mengi ambayo yanaweza kuambukizwa kwa kuongezewa damu kupitia njia isiyo salama. Tanzania na nchi nyingine zinazoendelea hutoa kipaumbele sana kwenye VVU, homa za ini na kaswende kutokana na kiwango cha maambukizi katika idadi ya watu. Haya magonjwa manne ni yote yanafanana na uambukizwa kupitia ngono na uongezwaji damu.

Maambukizi ya VVU na homa za ini husababishwa na virusi wakati kaswende husababishwa na bakteria. Watu walio athirika na virusi /vimelea vyovyote wanaweza kujisikia kuwa na afya njema, lakini wanaweza kusambaza maambukizi kwa mtu ambaye anapokea damu yao. vipimo vya damu vinaweza kutumika kwa uchunguzi wa hali ya maambukizi, ingawa matokeo yanaweza kuwa mabaya kwa wiki kadhaa baada ya kuambukizwa na virusi/vimelea.

Virusi/vimelea bado vinaweza kuambukizwa kwa mtu mwingine wakati huo. Kama ulipimwa na kukutwa na yoyote kati ya magonjwa haya manne, kufanya ngono ambayo ingehatarisha kuambukizwa virusi/vimelea au kuwa na historia ya magonjwa mengine ya kuambukiza, **USICHANGIE DAMU**. Yafuatayo ni mambo yanayoweza kukuweka katika hatari ya Kupata maambukizi ya Virus/vimelea, kama umetekeleza lolote kati ya haya, tafadhali **USICHANGIE DAMU**;

- Umekuwa na mpenzi mpya katika kipindi cha miezi 6 iliyopita.
- Ulikuwa na mpenzi zaidi ya moja katika kipindi cha miezi 6 iliyopita.
- Kama ni mwanaume uliyefanya ngono na mwanaume mwenzio katika kipindi cha miezi 6 iliyopita.
- Je, una mpenzi ambaye ana mpenzi/wapenzi wapenzi wengine zaidi yako katika kipindi cha miezi 6 iliyopita?
- Je, una historia ya kutumia dawa za kulevya katika kipindi cha miezi 6 iliyopita?
- Ulikuwa umejichora tattoo yoyote au kutoboa mwili, mfano kutoboa sikio katika miezi sita iliyopita?
- Kama ulishawahi kufanya ngono kwa kulipia au baada ya matumizi ya madawa ya kulevya
- Ndani ya miezi 12 iliyopita umefanya ngono na mtu ambaye alishawahi kushiriki katika shughuli yoyote ya kati ya hivyo vilivyotajwa hapo juu.
- Umewahi kuwa mhanga wa unyanyasaji wa kijinsia, mfano ubakaji au ulawiti? Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.
- Umepokea damu au damu bidhaa kwa sababu yoyote, ndani ya miezi 12 iliyopita.
- Umewahi kuwa na ugonjwa wa kuambukizwa (STD)?
- Umefanya ngono na mtu mwenye Ukimwi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita au ambaye aliyepima na kuonekana na virusi vya UKIMWI.
- Umepata jeraha la kumchomwa au kwa bahati mbaya uliumia kwa kujichoma na sindano au kitu chenye ncha kali katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.
- Ulikutana na mtu mwenye macho ya njano au ngozi njano katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.
- Ulikuwa na macho ya njano au ngozi njano katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.
- Ulishawahi kukutwa na homa ya ini kabla
- Umekutana na mtu mwenye homa ya ini au manjano katika kipindi cha mwaka mmoja uliyopita

Kama ulikuwa au ulishafanya hata moja ya mambo haya, basi umeongeza hatari ya kuwa na mambo hayo yaliyotajwa hapo juu na **HAUPASWI KUCHANGIA DAMU**. Damu yako itapimwa VVU, homa za ini na Kaswende na kama damu yako itagundulika kuwa na kwa yoyote kati ya magonjwa hayo manne utashauriwa kuripoti kituo cha afya kilichopo karibu nawe kwa ajili ya kupatiwa huduma na matibabu. Kama vipimo vya damu yako inaonyesha kwamba una VVU hutoruhusiwa kuchangia damu tena.

Kwa taarifa zaidi wasiliana: **Mpango wa Taifa wa Damu Salama**

S.L.P. 65019 Dar-es-Salam Tanzania. Simu: 0712612200 Barua Pepe: info@nbts.go.tz Tovuti: www.nbts.go.tz

Changia Damu, Okoa Maisha